# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## BUNGE LA TANZANIA

## KAMATI YA BUNGE YA BAJETI

# MAONI YA KAMATI KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO KWA MWAKA WA FEDHA 2019/20 PAMOJA NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/21

OFISI YA BUNGE
**DODOMA**
**15 Mei, 2020**

# YALIYOMO


**1.0. UTANGULIZI. .......... 4**

**2.0. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI NA MAJUKUMU YA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO PAMOJA NA OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI WA HESABU ZA SERIKALI KWA MWAKA WA FEDHA 2019/20 .......... 6**

**2.1. Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango**.......... 6

**2.2. Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali Fungu 45** 7

**2.3. Uchambuzi wa Kamati kuhusu Utekelezaji wa Bajeti kwa mafungu ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa Mwaka wa Fedha 2019/20.** .......... 11

**2.3.1. Fungu 07 - Ofisi ya Msajili wa Hazina**.......... 12

**2.3.2. Fungu 10 – Tume ya Pamoja ya Fedha** .......... 13

**2.3.3. Fungu 13 – Kitengo cha kudhibiti Fedha Haramu** .......... 13

**2.3.4. Fungu 21- Hazina** .......... 14

**2.3.5. Fungu 22 – Deni la Taifa na Huduma Nyingine** .......... 14

**2.3.6. Fungu 23- Mhasibu Mkuu wa Serikali**.......... 15

**2.3.7. Fungu 50 -Wizara ya Fedha na Mipango**.......... 15

**2.4. Uchambuzi wa Kamati kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Fungu 45 - Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2019/20.**.......... 16

**3.0. MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO PAMOJA NA OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI WA HESABU ZA SERIKALI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/21. .......... 19**

**3.1. Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mafungu 7 ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa Mwaka wa Fedha 2020/21.**.......... 19

**3.2. Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali (NAOT) kwa Mwaka wa Fedha 2020/21.** .......... 20

**4.0. MAONI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI YA BUNGE YA BAJETI .......... 21**

**4.1. Usimamizi wa Sera za kiuchumi (Fiscal policy) na Fedha (Monetary policy) katika kipindi cha janga la COVID -19** .......... 21

**4.2. Mfuko wa Majanga wa IMF na World Bank (*Catastrophic Containment Relief Fund*-CCRT)**.......... 22

**4.3. Ofisi ya Msajili wa Hazina** .......... 22

**4.4. Matumizi ya Mfumo wa TSA kwa upande wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar - SMZ** 23

**4.5. Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu**.......... 24

**4.6. Deni la Taifa na Huduma za Mfuko Mkuu**.......... 24

**4.7. Soko la Bidhaa Tanzania - TMX** .......... 24
**4.8. Mfumo wa Tathmini na Ufuatiliaji (M&E)** .......... 25
**4.9. Mifumo ya TEHAMA** .......... 26
**4.10. Mfumo wa Kodi za Kieletroniki *(Electronic Tax Stamp)*** .......... 26
**5.0. HITIMISHO .......... 28**

# MAONI YA KAMATI KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO KWA MWAKA WA FEDHA 2019/20 PAMOJA NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/21.

## 1.0. UTANGULIZI.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Bajeti kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka wa fedha 2019/20, pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2020/21 ambayo inajumuisha Mafungu Saba (7) ambayo ni Fungu 07 - Ofisi ya Msajili wa Hazina, Fungu 10 - Tume ya Pamoja ya Fedha, Fungu 13 - Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu, Fungu 21- Hazina, Fungu 22 - Deni la Taifa, Fungu 23 - Mhasibu Mkuu wa Serikali na Fungu 50 - Wizara ya Fedha na Mipango. Taarifa hii inajumuisha pia Fungu 45 – Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** moja ya jukumu la Kamati ya Bunge ya Bajeti kama yalivyoainishwa kwenye Nyongeza ya Nane kifungu cha 9 cha Kanuni za kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016 ni pamoja na kusimamia shughuli za Wizara ya Fedha na Mipango na taasisi zilizo chini ya Wizara hiyo. Aidha, kifungu cha 9 (1) (c) cha Sheria ya Bajeti Na. 11 ya mwaka 2015 pia kinaipa Kamati ya Bajeti jukumu la kupitia na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fungu – 45, Mfuko wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali. Kwa muktadha huo, katika nyakati tofauti, Kamati ilikutana na kufanya mashauriano na Serikali na hatimaye kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango na Mafungu yake yote Saba (7) pamoja na Fungu 45 - Mfuko wa Ofisi ya Taifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Fedha na Mipango ina jukumu la Kupanga Mipango ya Taifa na kusimamia utekelezaji Bajeti, sera za mapato na matumizi ya umma pamoja na sera za fedha na uchumi kwa ujumla. Majukumu hayo yanatekelezwa kupitia mafungu yaliyo chini yake kama ifuatavyo: -

i. Fungu 07 - Ofisi ya Msajili wa Hazina: Ofisi ya Msajili wa Hazina imepewa jukumu la kusimamia na kulinda rasilimali zilizowekezwa na Serikali katika Mashirika na Taasisi za Umma pamoja na Kampuni ambazo Serikali ina hisa. Majukumu ya Ofisi ya msajili ni kama yalivyobainishwa kwenye Sheria ya Msajili wa Hazina Sura Na. 370.

ii. Fungu 10 – Tume ya Pamoja ya Fedha: Tume ya Pamoja ya Fedha ni Taasisi ya Muungano wa Tanzania iliyoanzishwa kwa mujibu wa Ibara 134 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na baadae kuanzishwa kwa Sheria ya Tume ya Pamoja ya Fedha ya mwaka 1996, Sura 140. Jukumu kuu la Tume ni kuwa chombo cha ushauri kuhusiana na mambo yote ya Muungano yanayohusu fedha baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na majukumu mengine kama yalivyoainishwa kwenye Ibara ya 134(2) ya Katiba.

iii. Fungu 13 – Kitengo cha kudhibiti Fedha Haramu: Kitengo hiki ni chombo cha kiinteligensia kilichoanzishwa chini ya Sheria ya Udhibiti wa Fedha Haramu ya Mwaka 2006, Sura Na. 463 mahsusi kwa ajili ya kupambana na utakatishaji wa fedha haramu pamoja na ufadhili wa vitendo vya ugaidi nchini.

iv. Fungu 21- Hazina: Ofisi hii ina majukumu makuu matatu. Jukumu la **kwanza** ni kusimamia ukusanyaji wa mapato na matumizi ya fedha za Serikali, **Pili** ni kusimamia utekelezaji wa bajeti ya Serikali na **Tatu** ni

kusimamia Utekelezaji wa Sheria ya Mikopo na Dhamana ya Serikali Sura ya 137 ili kuhakikisha katika kipindi chote Deni la Serikali linaendelea kuwa himilivu.

v. Fungu 22 – Deni la Taifa: Idara hii inajukumu kubwa la kulipa madeni ya ndani na nje ya nchi (Principal debt) pamoja na riba (Interest). Aidha Idara hii pia inajishughulisha na mafao ya pensheni kwa wastaafu pamoja na michango ya mwajiri.

vi. Fungu 23- Mhasibu Mkuu wa Serikali: Idara hii ina jukumu la kusimamia matumizi ya fedha za Serikali na kutoa miongozo ya mifumo ya kifedha inayopaswa kutumiwa na taasisi zote za umma.

vii. Fungu 50 - Wizara ya Fedha na Mipango: Fungu hili linajukumu la msingi la kusimamia uchumi jumla kupitia sera za fedha (Fiscal Policy) na matumizi na mifumo ya kifedha kwa ajili ya kuimarisha ukuaji wa uchumi (Monetary Policy).

## 2.0. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI NA MAJUKUMU YA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO PAMOJA NA OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI WA HESABU ZA SERIKALI KWA MWAKA WA FEDHA 2019/20

### 2.1. Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa Fedha 2019/20, Wizara ya Fedha na Mipango iliidhinishiwa na Bunge kutumia jumla ya **shilingi 11,881,609,700,717** kwa mafungu yote saba (7) . Kati ya fedha hizo **Shilingi 11,157,327,758,988** zilikuwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambayo yanajumuisha malipo ya Deni la Taifa (pamoja na riba) **shilingi 4,899,168,000,000** Deni la Ndani, **Shilingi 2,963,410,000,000** kwa ajili ya Deni la Nje na **Shilingi 724,281,941,731** zilikuwa kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia mwezi Machi, 2020 jumla ya **shilingi 7,648,561,448,989** zilikuwa zimetolewa kwa Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na mafungu yake yote hii ikiwa ni sawa na **asilimia 64.37** ya Bajeti yote ya Wizara kwa kipindi husika. Kati ya fedha hizo **Shilingi 7,639,714,371,066** sawa na **asilimia 68.47** ya lengo zilikuwa ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **Shilingi 8,847,077,923** zilikuwa ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo sawa na **asilimia 1.22** tu ya Bajeti ya maendeleo.

## 2.2. Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali Fungu 45

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipitia Bajeti ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali ambapo kiasi cha **shilingi 62,142,554,000** zikihusisha fedha za maduhuli kwenda Mfuko Mkuu wa Serikali kiliidhinishwa kwa matumizi ya Ofisi hii katika mwaka 2019/20. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 55,076,878,000** zilikuwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida, **shilingi bilioni 6,300,000,000** zilikuwa kwa ajili ya matumizi ya maendeleo na **shilingi 765,676,000** ni fedha za makusanyo ya maduhuli.

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia mwezi Machi, 2020 lilikuwa limepokea kiasi cha **shilingi 46,431,843,915** sawa na **asilimia 75.65** Kati ya fedha hizo **shilingi 44,054,870,238** zilikuwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **Shilingi 2,376,973,677** zilikuwa kwa ajili ya matumizi ya maendeleo ambayo ni sawa na **asilimia 38** ya Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge. Aidha, jumla ya **shilingi 768,941,292** sawa na **asilimia 100.4** za maduhuli zilikuwa zimekusanywa na Ofisi.

Aidha, **Jedwali Na. 1** hapo chini linaonyesha mgawanyo wa bajeti kwa kila fungu pamoja na utekelezaji wa bajeti kwa kipindi cha robo tatu ya mwaka wa fedha 2019/20.

**Jedwali Namba 1. Utekelezaji wa Bajeti Kwa Mafungu ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka 2019/20**

| FUNGU | JINA LA FUNGU | BAJETI ILIYOIDHINISHWA 2019/20 | | FEDHA ILIYOTOLEWA HADI MACHI, 2020 | | ASILMIA YA FEDHA ZILIZOTOLEWA HADI APRILI, 2020 | | ASILIMIA KIASI CHOTE KILICHOTOLEWA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Matumizi ya kawaida | Maendeleo | Matumizi ya Kawaida | Maendeleo | Matumizi ya Kawaida | Maendeleo | (%) |
| 07 | Msajili wa Hazina | 40,510,802,000 | 2,300,000,000 | 9,778,470,300.67 | 450,934,700 | 24.1 | 19.6 | 23.9 |
| 10 | Tume ya Pamoja ya Fedha | 2,207,935,000 | - | 1,648,993,077 | - | 75 | 0 | 75 |
| 13 | Kitengo cha Udhibiti Fedha Haramu | 2,015,586,000 | 200,295,998 | 1,128,552,377 | 173,054,011.50 | 56 | 86 | 58 |
| 21 | Hazina | 1,272,801,249,988 | 683,717,888,733 | 353,304,655,576.43 | 3,211,169,240.44 | 27.76 | 0.47 | 18.22 |
| 22 | Deni la Taifa | 9,730,012,708,000 | - | 7,204,020,041,449.15 | - | 74.04 | 0 | 74.4 |
| 23 | Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali | 44,066,048,000 | 3,300,000,000 | 21,833,018,743 | 722,930,000 | 49.55 | 21.91 | 47.62 |
| 50 | Wizara ya Fedha na Mipango | 65,713,430,000 | 34,763,757,000 | 48,000,639,543 | 4,288,989,971 | 73 | 12 | 52 |
| **JUMLA** | | **11,157,327,758,988** | **724,281,941,731** | **7,639,714,371,066** | **8,847,077,923** | **68.47** | **1.22** | **64.37** |
| 45 | Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu ya Serikali | 55,076,878,000 | 6,300,000,000 | 44,054,870,238 | 2,376,973,677 | 80 | 38 | 76 |

**Jedwali Namba 2. Utekelezaji wa Bajeti ya Maendeleo Kwa Mafungu ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka 2019/20**

| FUNGU | JINA LA FUNGU | BAJETI YA MAENDELEO ILIYOIDHINISHWA 2019/20 | | FEDHA ILIYOTOLEWA HADI MACHI, 2020 | | ASILIMIA YA FEDHA ZILIZOTOLEWA | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Ndani | Nje | Ndani | Nje | Ndani | Nje |
| 07 | Msajili wa Hazina | 1,000,000,000 | 1,300,000,000 | 90,851,700 | 360,083,000 | 9.1 | 27.7 |
| 10 | Tume ya Pamoja ya Fedha | - | - | - | - | - | |
| 13 | Kitengo cha Udhibiti Fedha Haramu | - | 200,295,998 | - | 173,054,011.50 | 0 | 86 |
| 21 | Hazina | 656,000,000,000 | 27,717,888,733 | 137,005,000 | 3,074,164,240.44 | 0.02 | 11.09 |
| 22 | Deni la Taifa | - | - | | | | |
| 23 | Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali | 2,000,000,000 | 1,300,000,000 | - | 722,930,000 | 0 | 55.6 |
| 50 | Wizara ya Fedha na Mipango | 13,000,000,0000 | 21,763,757,000 | 2,196,828,476 | 2,092,161,495 | 17 | 10 |
| JUMLA | | 789,000,000,000 | 52,281,941,731 | 2,424,685,176 | 6,422,392,747 | 0.31 | 12.28 |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 45 | Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu ya Serikali | 5,000,000,000 | 1,300,000,000 | 1,471,148,677 | 905,825,000 | 29.4 | 70 |

## 2.3. Uchambuzi wa Kamati kuhusu Utekelezaji wa Bajeti kwa mafungu ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa Mwaka wa Fedha 2019/20.

### A: Uchambuzi wa Jumla.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Bajeti imefanya uchambuzi katika mafungu saba (7) yaliyo chini ya Wizara ya fedha na Mipango pamoja na **Fungu 45**- Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali. Kamati imebaini kuwa hadi kufikia mwezi Machi, 2020 :-

i. Mafungu **matatu 3** (**Fungu 10**- Tume ya Pamoja ya Fedha, **Fungu 22**- Deni la Taifa na **Fungu 50**- Wizara ya Fedha na Mipango) yalipokea zaidi ya **asilimia 60** ya fedha za matumizi ya kawaida zilizoidhinishwa na Bunge;

ii. Mafungu **mawili 2** (**Fungu 13** – Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu na **Fungu 23** – Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali) yalipokea zaidi ya **asilimia 50** ya bajeti nzima ya fedha za matumizi ya kawaida;

iii. Mafungu **mawili 2** (**Fungu 07** - Msajili wa Hazina na **Fungu 21**- Hazina) yalipokea chini ya **asilimia 30** ya fedha za matumizi ya kawaida; na

iv. Fungu **moja 1** (**Fungu 45**- Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali ilipokea zaidi ya **asilimia 60** ya fedha za matumizi ya kawaida zilizoidhinishwa na Bunge.

Aidha, kwa upande wa fedha za maendeleo, kati ya mafungu saba (7)**, ni mafungu mawili tu** yamepokea zaidi ya **asilimia 50** (**Fungu 13** – Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu na **Fungu 23** – Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali. Aidha, **Fungu 45** Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali ilipokea **asilimia 70** ya fedha za maendeleo. Mafungu mengine Matano yaliyobakia yalipokea fedha chini ya **asilimia 30**.

**Mheshimiwa Spika**, kwa takwimu hizi, utaona kuwa kati ya jumla ya **Shilingi 724,281,941,731** zilizoidhishwa na Bunge kwa Wizara kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo ni kiasi cha Shilingi **8,847,077,923 (**sawa na **asilimia 1.22)** ndiyo zimetolewa**.** Mwenendo huu sio wa kuridhisha ukizingatia kuwa miradi mingi ya maendeleo iliyochini ya Wizara ya Fedha na Mipango inahusu Maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma, uboreshaji wa mifumo ya kiuhasibu kwa njia za mtandao, uboreshaji wa mifumo ya ununuzi, utawala bora, ukarabati na ujenzi wa makazi. Hivyo, ni dhahiri miradi hii imeathirika kwa kiwango kikubwa hasa ukizingatia kuwa Serikali imekuwa haitoi mchango wake wa fedha za ndani (*local component*) kwenye miradi hii. Aidha, Washirika wa Maendeleo nao wamepunguza kasi ya kutoa fedha (*foreign component*) kwenye miradi hii.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ya Bajeti inapenda kutoa ushauri kwa Wizara ya Fedha na Mipango kuwa, kwa sasa Dunia nzima inajielekeza katika mapambano ya ugonjwa wa Covid-19, hivyo ni dhahiri misaada na mikopo ya masharti nafuu kutoka kwa washirika wa maendeleo itapungua.

## B: Uchambuzi wa Mafungu Mbalimbali.

### 2.3.1. Fungu 07 - Ofisi ya Msajili wa Hazina

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2019/20, Fungu hili liliidhinishiwa jumla ya **shilingi 42,810,802,000** hata hivyo hadi kufika mwezi Machi, 2020 kiasi cha **shilingi 10,229,405,00.67** ndicho kilikuwa kimetolewa na Hazina ikiwa ni sawa na asilimia **23.89** ya lengo.

**Mheshimiwa Spika,** utolewaji wa fedha kwa fungu hili umekuwa ni chini ya **asilimia 50** katika kipindi husika kwa miaka mitatu mfululizo**.** Mwenendo huu si wa kuridhisha hata kidogo na unaathiri matumizi maalum (special funds) ya urekebishaji wa mashirika ambayo ndiyo

yanayochukua kiasi kikubwa cha bajeti ya fungu hili. Hata hivyo kwa upande wa fedha za matumizi ya kawaida kwa ajili ya ofisi hii zimekuwa zikiongezeka na majukumu yamekuwa yakiongezeka na yanahitaji ongezeko zaidi la fedha za matumizi ya kawaida. Hivyo, Serikali lazima izingatie umuhimu wa majukumu ya Ofisi ya Msajili wa Hazina katika kusimamia rasilimali za Serikali.

#### 2.3.2. Fungu 10 – Tume ya Pamoja ya Fedha

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia mwezi Machi, 2020, Tume hii ilikuwa imepokea kiasi cha **shilingi 1,648,993,077** kati ya **shilingi 2,207,935,000** zilizoidhinishwa ikiwa ni sawa na **asilimia 74.68** ya bajeti yote ukiwa ni mwenendo mzuri wa utolewaji fedha kwa fungu hili.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuwa suala hili ni la muda mrefu, Kamati bado inaendelea kusisitiza juu ya ukamilishaji wa haraka wa mchakato wa ufunguaji wa Akaunti ya Fedha ya Pamoja (AFP) hasa ikizingatiwa kuwa tayari Muundo mpya ambao unaendana sambamba na majukumu ya Tume ulishapitishwa na mamlaka husika ya Serikali tangia mwezi Oktoba, 2018.

#### 2.3.3. Fungu 13 – Kitengo cha kudhibiti Fedha Haramu

**Mheshimiwa Spika,** hadi mwezi Machi, 2020 Kitengo kilikuwa kimepokea kiasi cha **shilingi 1,128,552,377** fedha kwa ajili ya matumizi ya kawaida ikiwa ni sawa na **asilimia 56.** Aidha, kwa upande wa fedha za maendeleo, Kitengo kiliidhinishiwa kutumia kiasi cha **shilingi 200,295,998 na** hadi kufikia mwezi Machi, 2020 kiasi cha **shilingi 173,054,011.50** kilikuwa kimepokelewa sawa na **asilimia 86** ya makadirio.

**Mheshimiwa Spika,** fedha hizi za maendeleo kwa fungu hili ni za nje, hivyo utekelezaji wake unategemea kwa kiasi kikubwa cha fedha kutoka kwa washirika wa maendeleo. Kamati inaishauri Serikali, kuanza

kufikiria kutenga fedha za ndani kwa ajili ya uendeshaji wa Kitengo cha kudhibiti Fedha Haramu ili kiweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo pasipo kutegemea fedha za wahisani hasa katika kipindi hiki cha janga la Corona.

### 2.3.4. Fungu 21- Hazina

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia mwezi Machi, 2020 Idara hii ilikuwa imepokea jumla ya **shilingi 356,515,824,816.87** sawa na **asilimia 18.22** ya bajeti yote iliyoidhinishwa na Bunge ya **shilingi 1,956,519,138,721**. Kwa upande wa fedha za maendeleo, Fungu hili limepokea kiasi cha **shilingi 3,211,169,240.44** kati ya **shilingi 683,717,888,733** sawa na **asilimia 0.47** ya fedha zote za maendeleo. Hali hii ni tofauti na ilivyokuwa kwa mwaka 2018/19 ambapo ilipokea kiasi cha **asilimia 85.2** ya fedha zote za maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inatambua kuwa mradi mkubwa wa maendeleo katika fungu hili ni ule unahusisha maboresho ya fedha za umma (PFMRP) ambao fedha zake nyingi zinatoka kwa wahisani. Hivyo imefikia wakati kwa Serikali kuanza kufikiri upatikanaji wa fedha za kutosha za ndani kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu, ukizingatia kuwa Idara hii ina umuhimu mkubwa katika kusimamia utekelezaji wa bajeti ya Serikali, sera, kanuni; kusimamia ukusanyaji wa mapato na matumizi ya fedha za Serikali; kufuatilia utekelezaji wa mipango ya maendeleo na mikakati ya kupunguza umaskini; kusimamia na kudhibiti Deni la Taifa.

### 2.3.5. Fungu 22 – Deni la Taifa na Huduma Nyingine

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2019/20 Fungu 22 liliidhinishiwa kutumia kiasi cha shilingi **9,730,012,708,000.** Hadi kufikia mwezi Aprili, 2020 Fungu hili lilikuwa limepokea jumla ya **shilingi 7,204,020,041,449.15** ikiwa ni sawa na **asilimia 74.04** ya lengo. Kati ya fedha hizo, kiasi kilichotolewa kwa ajili ya kugharamia deni la ndani ni

kiasi cha **shilingi 4,065,575,125,236.03** na deni la nje **shilingi 2,133,409,895,072.93** zote zikiwa sawa na **asilimia 86.05** ya fedha zote zilizotolewa. Kamati inaipongeza Serikali kwa kutoa fedha hizi ambazo pia zinasaidia kulipa mafao na pensheni kwa wastaafu wa Serikali wanaolipiwa Hazina pamoja na kulipa mirathi kwa warithi na malipo ya kiinua mgongo kwa watumishi wa Serikali walio kwenye mikataba

### 2.3.6. Fungu 23- Mhasibu Mkuu wa Serikali

**Mheshimiwa Spika,** Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali katika mwaka wa fedha 2019/20 iliidhinishiwa kutumia kiasi cha **shilingi 47,366,048,000**. Hadi kufikia mwezi Machi, 2020 Idara ilikuwa imepokea jumla ya **shilingi 22,555,948,743** ikiwa ni sawa na **asilimia 47.62**. Kati ya fedha hizo **shilingi 17,470,446,734** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo, **shilingi 4,362,572,009** kwa ajili ya mishahara na **shilingi 722,930,000** kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwa Idara. Kamati inasisitiza Idara hii kuendelea kusimamia ipasavyo majukumu yake hasa yale yanayohusu usimamizi wa Sera za Serikali zinazohusu ubora na usalama wa fedha na mali za serikali pamoja na usimamizi wa utekelzaji wa Sheria ya fedha ya Mwaka 2001 (kama ilivyorekebishwa mwaka 2004).

### 2.3.7. Fungu 50 -Wizara ya Fedha na Mipango

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2019/20 Fungu 50 – Wizara ya Fedha na Mipango liliidhinishiwa jumla ya **shilingi 100.477,187,000** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo. Hadi kufikia mwezi Machi, 2020 Wizara ilikua imepokea jumla ya **shilingi 52,289,629,514** sawa na **asilimia 52.04** ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo **shilingi 21,775,523,600** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo, **shilingi 26,225,115,943.01** kwa ajili ya mishahara na **shilingi 4,288,989,971** kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwa Idara na Taasisi zilizo chini ya fungu hili. Hatua hii imewezesha Kuratibu na kusimamia shughuli za

Bunge, Mipango na Bajeti ya Wizara pamoja na Kusimamia na kuratibu shughuli za taasisi na mashirika yaliyo chini ya Wizara.

### 2.4. Uchambuzi wa Kamati kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Fungu 45 - Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2019/20.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ya Bajeti ilikutana na Waziri wa Fedha na Mipango pamoja na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ili kufanya mashauriano kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fungu hili.

**Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali ni taasisi yenye jukumu la kufanya ukaguzi wa mapato na matumizi ya Serikali, kama yalivyoidhinishwa na Bunge. Kwa mujibu wa Hati ya Majukumu ya mwaka 2018, Ofisi imepewa majukumu yafuatayo:

i. Kukagua hesabu za Wizara, Mikoa, Halmshauri za Wilaya, Miji, Manispaa na Majiji, Ofisi za Balozi za Tanzania zilizoko nje ya nchi, Wakala za Serikali, Mashirika ya Umma, pamoja na Miradi ya Maendeleo inayogharamiwa na wafadhili na kutoa taarifa ya ukaguzi huo Bungeni juu ya mapato na matumizi ya fedha za Umma;
ii. Kujenga, kukuza na kuimarisha utamaduni wa uwajibikaji katika Wizara na Taasisi za Serikali, Mikoa na Halmshauri;
iii. Kuhakikisha kwamba, inajiridhisha kuwa upo uwajibikaji wa kutosha katika kusimamia na kudhibiti ipasayo ukusanyaji wa mapato na matumizi ya Serikali; na
iv. Kuhakikisha kuwa jamii ya Tanzania inapata faida au tija kutokana na matumizi bora ya fedha za Umma, na mali za Umma zinahifadhiwa, kutunzwa na kulindwa ipasavyo.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2019/20 Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali iliidhinishiwa jumla ya kiasi cha **Shilingi 61,376,878,000** kutoka Mfuko Mkuu kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Kati ya fedha hizo mishahara ni **Shilingi 14,084,139,000** matumizi mengineyo (OC) **Shilingi 40,992,739,000** na **Shilingi 6,300,000,000** zilitengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ambapo fedha za ndani zilikuwa **shilingi 5,000,000,000** na **shilingi 1,300,000,000** ni fedha za nje. Kwa upande wa maduhuli, Ofisi ilikadiriwa kukusanya kiasi cha **shilingi 765,676,000.** Maduhuli ya Ofisi hii yanatokana na marejesho ya gharama za ukaguzi (reimbursable costs) wa Mashirika ya Umma, ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo inayosimamiwa na Wizara chini ya Divisheni ya Serikali Kuu pamoja na ile ya miradi chini ya Divisheni ya Hesabu za Taifa.

**Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza Bajeti hiyo hadi kufikia mwezi Machi, 2019 Ofisi ilikuwa imepokea jumla ya kiasi cha **shilingi 46,431,843,915** kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali. Kiasi hicho ni sawa na **asilimia 75.65**. Kati ya kiasi hicho, **shilingi 9,024,969,571** ni kwa ajili ya mishahara, **Shilingi 32,161,747,099** ni kwa Matumizi ya mengineyo na shilingi **shilingi 2,060,123,677** ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo**.**

**Mheshimiwa Spika,** kiasi hicho cha bajeti kilichotolewa kimeiwezesha Ofisi kutekeleza shughuli mbalimbali zilizokuwa zimepangwa kulingana na fedha zilizopokelewa kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali na makusanyo ya ndani. Aidha, mwenendo wa utolewaji wa fedha kutoka Mfuko Mkuu kwa Ofisi kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo umebaki kuwa wa changamoto ambapo hadi kufikia mwezi Machi, 2019 kiasi kilichokuwa kimepokelewa ni **asilimia 38** tu ya makadirio. Hivyo ni vema Serikali ikaangalia namna ya kuongeza bajeti ya maendeleo katika Ofisi hii.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilifanya tathmini ya mwenendo wa sura ya bajeti ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi za Hesabu za Serikali iliyokuwa inatengewa na Serikali kwa kipindi cha miaka 4 kuanzia 2017/18 hadi 2020/21. Bajeti ya Fungu 45 ilianza kushuka katika mwaka 2017/18 hadi 2019/20 ikilinganishwa na bajeti inayoombewa mwaka 2020/21. Aidha, mwaka 2020/21 bajeti ya NAOT imeongezeka kwa **asilimia 31.** Kamati inaipongeza Serikali kwa kuongeza bajeti ya ofisi hii muhimu.

**Mheshimiwa Spika,** kwa ujumla bajeti ya mwaka 2020/21 imeongezeka kwa jumla ya **shilingi 19,168,057,373** ukilinganisha na ile ya mwaka 2019/20. Kati ya kiasi kilichoongezeka fedha za matumizi mengineyo zimeongezeka kwa **shilingi 13,001,000,373** na matumizi ya maendeleo yameongezeka kwa **shilingi 5,367,940,000**. Aidha, ongezeko hili limepelekea pia kuongezeka kwa mawanda ya ukaguzi ambazo awali yalikuwa hayafanyiki kutokana na ukosefu wa fedha pamoja na mambo mengine.

**Mheshimiwa Spika**, ongezeko la bajeti ya NAOT ni kiashiria kizuri kwa upande wa uhuru wa Ofisi ya CAG kwa kuzingatia vigezo vya kimataifa. Aidha, bado Ofisi ya CAG ina changamoto ya kutokuwa na kibali cha kuajiri watumishi wake mwenyewe. Hali ilivyo watumishi wa Ofisi hii wanajiriwa kupitia Ofisi ya Utumishi ambavyo ni kinyume na vigezo vya uhuru wa CAG vilivyowekwa kimataifa. Hivyo, ni ushauri wa Kamati kuwa Serikali izingatie Sheria na majukumu ya Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, ungezeko la fedha hizi zitasaidia kutatua baadhi ya changamoto zifuatazo :-

i. Kuongeza mawanda ya ukaguzi na kufikia maeneo ambayo Ofisi inaona yana viashiria vya mwenendo wenye shaka katika mapato na matumizi ya fedha za Serikali;

ii. Kukagua miradi mikubwa ya Maendeleo ya Kimkakati inayotekelezwa na Serikali yenye mahitaji makubwa ya kibajeti ya ukaguzi wa maeneo hayo. Hii ni pamoja na hitaji I kufanya ukaguzi wa kiufundi na thamani ya fedha katika miradi hiyo ili kujiridhisha kuwa Serikali inapata matokeo tarajiwa;
iii. Kufanya ukaguzi unaohitajika kwa kiwango cha kimataifa kwenye mifumo ya TEHAMA ya Serikali inayohusika na ukusanyaji wa mapato na matumizi ya Serikali;
iv. Kuongeza ukaguzi kwenye mahitaji maalum ya ukaguzi katika ngazi ya Serikali Kuu, Serikali za Mitaa, Mashirika ya Umma, Bunge na Mahakama; na
v. Kununua vitendea kazi muhimu pamoja na ukarabati wa majengo ya ya Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (NAOT).

## 3.0. MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO PAMOJA NA OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI WA HESABU ZA SERIKALI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/21.

### 3.1. Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mafungu 7 ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa Mwaka wa Fedha 2020/21.

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2020/21 imekadiriwa kutumia jumla ya **Shilingi 12,402,962,303,000** kwa mafungu yote Saba (7). Kati ya fedha hizo, **Shilingi 11,228,096,030,000** ni kwa ajili ya Matumizi mengineyo (OC) na kwa ajili ya kulipia Deni la Serikali (ndani na nje) kiasi cha **shilingi 8,649,941,441,000**, **shilingi 510,045,950,000** ajili ya mishahara na **Shilingi 664,820,323,000** ni kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo inayotarajiwa kutekelezwa na Wizara katika kipindi husika.

### 3.2. Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali (NAOT) kwa Mwaka wa Fedha 2020/21.

**Mheshimiwa Spika**, Ofisi kwa mwaka wa fedha 2020/21 imelenga kuimarisha ukaguzi wa mapato na matumizi ya Serikali kwa lengo la kuimarisha uwajibikaji na uwazi kwenye matumizi ya rasilimali za umma ambapo imepanga kutumia **shilingi 80,544,935,000** kwa kuzingatia vipaumbele na kazi za Ofisi zilizolengwa kutekelezwa. Kati ya fedha hizo, **shilingi 14,883,256,000** ni kwa ajili ya matumizi ya mishahara; **shilingi 53,993,739,000** matumizi mengineyo na **shilingi 11,667,940,000** ni jumla ya fedha za maendeleo za ndani na nje.

**Mheshimiwa Spika**, kama tulivyosema hapo awali kuwa bajeti hii imeongezeka kwa **asilimia 31** ikilinganishwa na bajeti ya mwaka 2019/20. Aidha, fedha hizo zinajumuisha nyongeza ya fedha ya **shilingi 14,800,00,000** kutoka Wizara ya Fedha na Mipango kati ya **shilingi 20,000,000,000** zilizokuwa zimeombwa nje ya ukomo wa bajeti. Ni matumaini ya Kamati kuwa Fungu 45 litaendelea kupatitiwa fedha kulingana na mahitaji yake ili iweze kutekeleza majukumu yake ya kikatiba.

**Jedwali Namba 4. Maombi ya Fedha Kwa Wizara ya Fedha na Mipango na Mafungu yaliyo Chini Wizara Pamoja na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali kwa Mwaka 2020/21.**

| FUNGU | MATUMIZI MENGINEYO (OC) | MISHAHARA | MIRADI YA MAENDELEO | JUMLA |
|---|---|---|---|---|
| 07 | 22,229,786,000 | 3,375,080,000 | 2,300,000,000 | 27,904,866,000 |
| 10 | 2,048,142,000 | 802,823,000 | - | 2,850,965,000 |
| 13 | 2,915,586,000 | - | 500,000,000 | 3,415,586,000 |
| 21 | 637,275,862,000 | 450,901,950,000 | 641,000,892,000 | 1,729,178,704,000 |
| 22 | 10,477,797,406,000 | 9,989,416,000 | - | 10,487,786,822,000 |
| 23 | 58,036,734,000 | 5,738,683,000 | 3,500,000,000 | 67,275,417,000 |
| 50 | 27,792,514,000 | 39,237,998,000 | 12,016,431,000 | 79,046,943,000 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **JUMLA** | **11,228,096,030,000** | **510,045,950,000** | **664,820,323,000** | **12,402,962,303,000** |
| **45** | 53,993,739,000 | 14,883,256,000 | 11,667,940,000 | 80,544,935,000 |
| **JUMLA KUU** | **11,282,089,769,000** | **524,929,206,000** | **676,488,263,000** | **12,483,507,238,000** |

## 4.0. MAONI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI YA BUNGE YA BAJETI

**Mheshimiwa Spika,** baada ya Kamati kupitia utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha 2019/20 pamoja na mapato na matumizi ya mafungu husika kwa mwaka wa fedha 2020/21; Kamati inapenda kutoa **maoni na mapendekezo** yake kama ifuatavyo: -

### 4.1. Usimamizi wa Sera za kiuchumi (Fiscal policy) na Fedha (Monetary policy) katika kipindi cha janga la COVID -19

**Mheshimiwa Spika**, moja ya jukumu kubwa la Wizara ya Fedha na Mipango ni Kuimarisha ukuaji wa uchumi jumuishi na endelevu kupitia sera bora za uchumi kwa maendeleo ya watu pamoja na ukusanyaji wa mapato ya Serikali. Kamati inatoa ushauri kwa Wizara ya Fedha na Mipango kuanza kufikiria namna ya kupanga sera zake za kiuchumi katika kipindi cha muda mfupi, wa kati na mrefu ili kusaidia kutatua matatizo ya kiuchumi yatokanayo na COVID -19.

**Mheshimiwa Spika,** ni dhahiri kuwa COVID -19 imeathiri mtu mmoja mmoja, kaya na biashara zote kwa ujumla na hivyo hali hii inaleta usumbufu wa utekelezaji shughuli za uchumi na pia imeathiri msingi wa maoteo ya mapato (*revenue forecasting*), ulipaji na usimamizi wa kodi na mwenendo wa uchumi. Hivyo kuna umuhimu wa Wizara hii kulazimika kufanya maamuzi muhimu ya sera kulingana na mazingira ya sasa kwa maendeleo ya watu pamoja na ukusanyaji wa mapato.

**Mheshimiwa Spika**, aidha, Kamati inaipongeza Serikali kupitia Benki Kuu, imeanza kuchukua hatua za udhibiti wa sekta ya fedha na upatikanaji wa huduma ya fedha katika shughuli za kiuchumi. Hatua za kushusha kiwango cha *Statutory Minimum Reserve* - SMR kutoka asilimia 7 hadi asilimia 6, kushusha kiwango cha riba ya kukopeshana kati ya mabenki na mabenki kutoka asilimia 7 hadi 5 pamoja na kuongeza unafuu kwenye dhamana na hati fungani za serikali. Ni matumaini ya Kamati kuwa hatua hizi pia zitaenda kuwanufaisha na kuwasiaidi wakopaji wa kawaida, taasisi na makampuni binafsi watakaokopa. Kamati inaishauri Wizara ya Fedha na Mipango kupitia Benki Kuu kusimamia zoezi hili kwa mabenki ili lilete tija katika ukuaji wa uchumi.

### 4.2. Mfuko wa Majanga wa IMF na World Bank (*Catastrophic Containment Relief Fund*-CCRT)

**Mheshimiwa Spika**, itakumbukwa hivi karibuni Shirika la Fedha Duniani (IMF) pamoja na Benki ya Dunia zimetoa ahueni ya kulipa madeni pamoja na Msaada kupitia Mfuko wa CCRT wa kukabiliana na Majanga. Tumeshuhudia nchi jirani za Afrika mashariki, Magharibi na Kusini mwa Afrika zikipokea fedha kwa ajili ya kupambana na janga la corona pamoja na kusaidia sekta mbalimbali kupambana na mdororo wa uchumi. Kamati inaishauri Serikali kuangalia uwezekano wa kupata fedha hizo ili ziweze kusaidia kukabiliana na athari zinazotokana na janga la COVID-19. Uwezekano huo uangaliwe kwa kuzingatia faida na hasara za ahueni hiyo pamoja na kuzingatia Sheria ya Mikopo na Dhamana ya Serikali Sura ya 137.

### 4.3. Ofisi ya Msajili wa Hazina

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na bajeti ya Fungu 7 kushuka kwa **asilimia 34.8** kwa mwaka wa fedha 2020/21, fungu hilo limeongezewa

majukumu ya kusimamia Viwanda na Mashamba yaliyobinafsishwa na yaliyorejeshwa Serikalini ambapo kimsingi imeiongezea Ofisi gharama kwa ajili ya kuvitunza viwanda na mashamba hayo. Kamati inashauri Serikali kuhakikisha kuwa Ofisi hii inapatiwa fedha za kutosha ili kukabiliana na majukumu iliyoongezewa. Vilevile, Kamati inashauri Serikali kuja na mkakati wa haraka wa kuendeleza mashamba, viwanda na mali zilizoreshejwa Serikalini ili kuipunguzia Serikali mzigo wa gharama wa kutunza rasilimali hizo.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na hayo, Kamati inasisitiza kuwa Serikali itekeleze yafuatayo: **kwanza**, kuwekeza katika yale mashirika ambayo ina umiliki mdogo (*minority shareholding*); **pili**, inapata *return* ya uwekezaji uliofanywa kwenye Mashirika hayo; na **tatu**, Serikali iangalie njia mbadala ya upatikanaji wa mitaji kwa mashirika yenye uhitaji mathalani kupitia Soko la Hisa (DSE) na sio kutegemea fedha kutoka Serikali Kuu.

### 4.4. Matumizi ya Mfumo wa TSA kwa upande wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar - SMZ

**Mheshimwa Spika,** Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar bado haijaanza kutumia mfumo wa Akaunti Jumuifu ya Fedha (TSA) kutokana na kuwa pindi mfumo huu wakati unaanzishwa; SMZ ilikuwa haijakidhi vigenzo muhimu ikiwa pamoja na mifumo ya malipo ya kielektroniki. Aina ya mifumo hii ya malipo na mingine ndio ambayo ipo kieletroniki itawezesha SMZ kupata mapato sahihi. Hivyo ni wajibu wa Serikali kuchukua suala hili kwa uzito wake ili kuhakikisha kuwa pande zote mbili za Muungano zinatumia mifumo inayosomana ikizingatiwa masuala ya kifedha ni ya kimuungano lakini pia ili Akaunti ya Pamoja ya Fedha iweze kufanya kazi kwa ufanisi pindi itakapofunguliwa.

## 4.5. Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu

**Mheshimiwa Spika,** kuna haja ya kitengo kuangalia upya majukumu yake kwa sababu yanaonyesha jukumu lao kubwa ni kupoakea na kuchambua Taarifa kwa maana nyingine wanakuwa *reactive* kuliko *proactive*. Ina maana kunapotokea watoa Taarifa hawajaleta Taarifa kitengo kitakuwa na kazi chache za kufanya. Ni vyema Kitengo hiki ikawa na mifumo ya mawasiliano itakayohakikisha upatikananji wa taarifa na takwimu sahihi za miamala ya malipo ili kubaini maeneo yenye viashiria vya utakatishaji wa fedha.

## 4.6. Deni la Taifa na Huduma za Mfuko Mkuu

**Mheshimiwa Spika,** Fungu 22 pamoja na kuhudumia deni la Taifa pia linatoa huduma nyingine za Mfuko Mkuu wa Serikali ikiwa ni pamoja na malipo ya pensheni, michango ya mwajiri, bima ya afya na mishahara ya viongozi na maafisa wa umma na kiinua mgongo kwa baadhi ya viongozi. Matumizi hayo yanaongeza fedha kwa Fungu hili kuonekana kubwa na kwa Tafsiri ya Deni kuonesha malipo ya Deni yanakuwa kwa kasi wakati nyingine ni stahili za Viongozi na Watumishi wa Umma.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inashauri Serikali, Fungu hili liwe ni maalumu kwa ajili ya masuala yote ya madeni tu na hayo matumizi mengine yanaweza kuhamishiwa katika Idara na Taasisi za Serikali kama Utumishi, Mfuko wa Mahakama na mafungu mengine. Hatua hii ni ya busara kwa kuwa itaipa uzito wa kipekee fedha zinazotengwa kwa ajili ya kugharamia Deni la Taifa.

## 4.7. Soko la Bidhaa Tanzania - TMX

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inatambua umuhimu wa kuanza kutumika rasmi kwa soko la bidhaa – TMX lakini bado soko hili halijaweza kuwa na mifumo madhubuti itakayowezesha TMX kufanya kazi kwa ufanisi. Mfumo unaongelewa hapa, ni mfumo wa stakabadhi ghalani ambao

sio mazao yote yana mfumo huu. Hata hivyo, mfumo huu unataka kuwepo kwa miundombinu wezeshi kama, mfumo wa ununuzi (vyama vya ushirika) na maghala ya kutosha nchini yatakayoweza kukidhi mahitaji ya soko na kuongeza ufanisi wa Mfumo wa stakabadhi za ghala.

**Mheshimiiwa Spika,** Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuhakikisha uwepo wa miundombinu hiyo wezeshi, kuwa na mfumo wa utoaji taarifa sahii za bei na masoko na usimamizi wa Soko lenyewe.

### 4.8. Mfumo wa Tathmini na Ufuatiliaji (M&E)

**Mheshimiwa Spika,** moja ya jukumu la Wizara ya Fedha na Mipango ni pamoja na kufuatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa na Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala, Taasisi za Umma, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Sekta Binafsi. Aidha, bado kuna changamoto katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo inayotokana na kutokufanyika kwa tathmini na utekelezaji wa miradi hii kwa ufanisi.

**Mheshimiwa Spika**, miradi mingi ya maendeleo imekuwa na mapungufu makubwa, mingine kutokukamilika kabisa na mengine kutekelezwa miradi hewa. Hii ni dhahiri kuwa suala la M&E limekuwa halitekelezeki na hivyo kuipelekea nchi hasara kubwa. Hivyo, ni vema Serikali ikalichukulia suala hili kwa uzito wake na kuleta uwajibikaji katika Serikali na kuzingatia utaalamu katika kusimamia miradi. Aidha, hatua hii iendane sambamba na uanzishwaji wa Sera ya Taifa ya Ufuatiliaji na Tathmini pamoja na ukamilikaji wa mfumo wa kitaifa wa ufuatiliji na tathmini ya miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** vilevile maboresho haya yaende sambamba na uwepo wa uhuru wa wakaguzi wa ndani wa Serikali Kuu, Halmashauri na Mamlaka za Serikali za Mitaa tofauti na ilivyo hivi sasa.

### 4.9. Mifumo ya TEHAMA

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na juhudi nzuri zinazofanywa na Wizara katika ubunifu wa mifumo mbali mbali ya TEHAMA, kumekuwa na uanzishwaji wa mifumo mingi nchini na hivyo kupelekea kuwepo na utitiri wa mifumo ambayo mingine inafanya kazi zinazoshabihiana. Ni ushauri wa Kamati kuwa, Serikali iwe na mfumo mmoja na kuanzisha *modules* badala ya mifumo mipya ili kushughulikia masuala mapya pamoja na kuihisha mifumo iliyopo ili isomane.

### 4.10. Mfumo wa Kodi za Kieletroniki *(Electronic Tax Stamp)*

**Mheshimiwa Spika,** moja ya mabadiliko makubwa yaliyofanywa na Serikali ni kuanzisha mfumo wa Stempu za Kodi za Kieletroniki. Mfumo huu unasaidia kutambua bidhaa halisi (*Genuine*) na bidhaa ambazo hazina ubora katika soko. Aidha, mfumo huu unaisaidia mamlaka ya Mapato kukadiria Kodi Stahiki na mlaji kutambua kama bidhaa anayotumia ni halisi ama la. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuangalia uwezekano wa mfumo huo kutumika katika bidhaa nyingine za viwandani ambazo zinamfumo unaowezesha stempu hizo kuwekwa ili kupata mapato sahihi kutoka bidhaa hizo. Aidha, mfumo huo unaweza kutumika katika utambuzi wa pembejeo ili kuwasaidia wakulima wetu ambao wamekuwa wakiathirika na uzalishaji, uingizaji na usambazaji wa pembejeo zisizo na ubora.

### 4.11. Uhakiki na Ulipaji wa Madeni ya Watumishi, Wakandarasi na Wazabuni.

**Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Februari, 2020 Serikali ilikuwa imekwisha kulipa jumla ya **shilingi 327,804,805,268.56** kwa ajili ya madeni ya Wakandarasi, Wazabuni na Watoa Huduma

yaliyohakikiwa. Kati ya fedha hizo Wakandarasi walilipwa **shilingi 14,667,577,422.21**, Watumishi **shilingi 60,717,890,332.16,** Wazabuni **shilingi 147,731,394,644.53**, Watoa Huduma **shilingi 15,813,720,395.85** na madeni mengineyo kama vile fidia na michango ya kimataifa **shilingi 88,874,222,203.81**.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa jitihada za kuendelea kuhakiki na kulipa madeni hayo. Hata hivyo, kwa kuwa suala hili ni la muda mrefu na madeni mapya yanaendelea kuzalishwa, Kamati inaendelea kuisistizia Serikali inahakikisha inaendelea na ulipaji wa madeni yote yaliyohakikiwa ili kupunguza gharama kwa Serikali hasa kwa madeni yenye ongezeko la riba lakini pia gharama kwa watoa huduma waliokopa kwenye mabenki kupata mtaji ili waweze kutoa huduma kwa Serikali. Suala hili la ulipaji wa madeni ni muhimu hasa katika kipindi hiki cha ugonjwa wa Covid-19. Hatua hii itasaidia kuongeza ukwasi kwenye uchumi ili kusaidia biashara zisife na kupunguza mikopo chechefu katika mabenki ya ndani ambayo Wafanyabiashara wengi wa ndani walikopa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilibaini kuwepo na changamoto ya hati za madai za wakandarasi kutoka wizara na taasisi nyingine zinazowasilishwa Hazina kwa ajili ya malipo. Hati hizo zimeonekana kuwa na upungufu na suala hili limekuwa linajirudia mara kjwa mara na hivyo kupelekea kuchelewa kwa malipo hayo. Kamati inaitaka Serikali kurejea Waraka Na 1 kuhusu Utekelezaji wa Bajeti na Waraka namba 3 kuhusu uhakiki na ulipaji wa madeni wa mwaka 2019 ambao unatoa muongozo kwa Maafisa masuuli wa namna ya kufanya manunuzi na kuwasilisha nyaraka mbalimbali za madeni ili ziweze kuhakikiwa na kulipwa. Hali ilivyo hivi sasa Nyaraka hizo zinajulikana na kutumika zaidi

na Wizara ya Fedha peke yake kuliko maafisa masuuli wa wiazra na taasisi nyingine.

## 5.0. HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** naomba nihitimishe kwa kukushukuru wewe Mhe. Spika, Dkt. Tulia Akson, Mb - Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa miongozo yenu ambayo mmekuwa mkitupatia. Shukrani pia ziwaendee Mhe. Dkt Philip Mpango (Mb) Waziri wa Fedha na Mipango, Mhe. Dkt Ashatu K. Kijaji (Mb), Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Katibu Mkuu na Naibu Makatibu Wakuu pamoja na wataalamu wote wa Wizara ya Fedha na Mipango kwa ushirikiano wao mkubwa waliotupa wakati wote wa kujadili utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Aidha, Kamati inatoa shukrani kwa Wakuu wa Taasisi na Idara zote zilizo chini ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa ushirikiano na ufafanuzi walioutoa kwa Kamati katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee kabisa napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati kwa umahiri, umakini na ushirikiano wao walionipatia wakati wote wa kuchambua bajeti ya Wizara hii na hatimaye kukamilika kwa taarifa hii. Aidha, naomba niwatambue Wajumbe wa Kamati kwa majina yao kama ifuatavyo: -

1. Mhe. Mashimba Mashauri Ndaki, Mb – M/Mwenyekiti
2. Mhe. David Ernest Silinde, Mb
3. Mhe. Mbaraka Kitwana Dau, Mb
4. Mhe. Mendrad Lutengano Kigola, Mb
5. Mhe. Maria Ndilla Kangoye, Mb
6. Mhe. Dkt. Immaculate Swale Semesi, Mb

7. Mhe. Ali Hassan Omar, Mb
8. Mhe. Freeman Aikael Mbowe, Mb
9. Mhe. Martha Jachi Umbulla, Mb
10. Mhe. Makame Kassim Makame, Mb
11. Mhe. Dkt. Dalaly Peter Kafumu, Mb
12. Mhe. Albert Obama Ntabaliba, Mb
13. Mhe. Oran Manase Njeza, Mb
14. Mhe. Riziki Said Lulida, Mb
15. Mhe. Hasna Sadi Katunda Mwilima, Mb
16. Mhe. Balozi Adadi Mohamed Rajabu, Mb
17. Mhe. Abdallah Majurah Bulembo, Mb
18. Mhe. Prof. Anna Kajumulo Tibaijuka, Mb
19. Mhe. Stephen Julius Masele, Mb
20. Mhe. Marwa Ryoba Chacha, Mb
21. Mhe. Dkt. Balozi Diodorus Buberwa Kamala, Mb
22. Mhe. Joseph George Kakunda, Mb
23. Mhe. John Kibera Kishimba, Mb
24. Mhe. Andrew John Chenge, Mb
25. Mhe. Shally Josepha Raymond, Mb
26. Mhe. Suleiman Ahmed Saddiq, Mb
27. Mhe. Dkt. Raphael Masunga Chegeni, Mb

**Mheshimiwa Spika,** mwisho naomba nitoe shukrani zangu za dhati kwa Katibu wa Bunge, Ndugu Stephen Kagaigai pamoja na watendaji wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Aidha, kwa

namna ya pekee napenda kuishukuru Sekretarieti ya Kamati ya Bajeti ikiongozwa na Mkururgenzi wa Bajeti Ndugu Michael Kadebe kwa kuratibu shughuli za Kamati pamoja na kutoa ushauri wa kitaalamu na hatimaye kukamilika kwa taarifa hii kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo naliomba Bunge lako tukufu sasa lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na mafungu manane (8) yaliyo chini yake kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 kama yalivyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

Mashimba M. Ndaki, Mb

**M/MWENYEKITI**
**KAMATI YA BUNGE YA BAJETI**

15 Mei, 2020